

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA IGUNGA

SHULE YA SEKONDARI MWISI,
S.L,P 173,
IGUNGA.
09/12/2020
SIMU:0767 066 073

Kumb. Na. MSS/J/VOL.1/19

Ndugu.....

S/M.....

YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWISI KIDATO CHA KWANZA - 2021

Husika na kichwa cha habari hapo juu. Ninayofuraha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kуjiunga na masomo ya sekondari kidato cha kwanza katika shule yetu ya Mwisi Sekondari. Natoa pongezi kwako kwa kupata nafasi hii muhimu katika maisha ya binadamu. Ni imani yangu kubwa kuwa utaitumia nafasi hii vizuri katika kufanikisha lengo lako binafsi na la taifa kwa ujumla.

Shule ya sekondari Mwisi ni ya kutwa inayomilikiwa na Serikali kuitia wananchi. Ipo wilaya ya Igunga mkoani Tabora. Kwa sababu shule hii ni ya kutwa Mzazi/Mlezi atawajibika kumtafutia kijana wake malazi pamoja na chakula wakati wote akiwa shulenii.

Pia shule ina hosteli kwa ajili ya wanafunzi wa kike. Kwa jinsi ya kуjiunga na Hostel pamoja na kupata huduma ya chakula kwa wanafunzi wa kutwa wasiliana na

Mkuu wa shule mapema kwa namba za simu hapo juu.

KUFUNGUA SHULE

Shule itafunguliwa **tarehe 11/01/2021**, unatakiwa kuripoti tarehe hiyo kwani **Form One English Orientation Course** itaanza siku hiyo. Endapo hutarioti tarehe hiyo hatua Kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yako na mzazi wako kuitia ofisi ya Kata.

Pamoja na barua hii, naambatanisha fomu mbalimbali zinazotoa taarifa za kуjiunga na shule yetu. Baadhi ya fomu husika zinatakiwa zijazwe na kurejeshwa shulenii siku ya kuripoti ambazo ni fomu **C, D, E** na **F**.

MUHIMU:

Ni lazima kila mwanafunzi aje na daftari kubwa kumi (Counter book Quire 3), Mathematical set, Kitabu cha kiingereza kiitwacho “Mabala the Farmer” na Kamusi ya kiingereza kwa kiingereza (English dictionary) kwa ajili yake binafsi.

Nakutakia masomo mema na karibu sana Mwisi Sekondari.

Wako katika Elimu

.....
MUNKUNDA ABDULLAH M.

MKUU WA SHULE

KIAMBATISHO A: MAELEKEZO VA KUJIUNGA NA SHULE

1. SARE ZA SHULE

WASICHANA

- ❖ Sketi 2 za rangi ya kijivu ambazo atashona mwenyewe, hakikisha Inavuka magoti (katikati ya goti na jicho la mguu) iwe na marinda kuanzia 10 na kuendelea na iwe ya heshima.
- ❖ Mashati mawili ya tetroni mikono mifupi.
- ❖ Viatu vya ngozi vya kamba na vinavyopigwa kiwi, visiwe na urembo na ziwe jozi mbili.
- ❖ Soksi ndefu nyeupe (stockings) jozi mbili.
- ❖ Tai ndefu za rangi ya kijivu jozi mbili zenyenye upana wa sentimeta 4.5
- ❖ Sketi 2 za light blue kwa ajili ya kuvalaa jioni atashona mwenyewe, hakikisha inavuka magoti na iwe na marinda kuanzia 10 na kuendelea
- ❖ Sweta la blue lenye V - shape la kuvalaa wakati wa baridi
- ❖ Aje na bima ya afya au kadi ya **CHF** kwa ajili ya matibabu na aje na passport size 4

WAVULANA

- ❖ Suruali 2 za rangi ya kijivu ambazo atashona mwenyewe, hakikisha inakuwa na marinda 2 kila upande, iwe pana na ya heshima yenye mifuko 2 mbele na 1 nyuma.
- ❖ Mashati mawili ya tetroni mikono mifupi.
- ❖ Viatu vyeusi vya ngozi vya kamba na vinavyopigwa kiwi, visiwe na urembo jozi mbili.
- ❖ Soksi nyeupe jozi mbili.
- ❖ Tai ndefu za rangi ya kijivu jozi mbili zenyenye Upana wa sentimeta 4.5
- ❖ Suruali mbili za light blue kwa a jili ya kuvalaa jioni atashona mwenyewe, hakikisha iwe na marinda mawili kila upande, iwe na mifuko 2 mbele na 1 nyuma.
- ❖ Sweta la blue lenye V - shape la kuvalaa wakati wa baridi.
- ❖ Aje na bima ya afya au kadi ya **CHF** kwa ajili ya matibabu na aje na passport size 4.

2. SARE ZA MICHEZO KWA WOTE

- ❖ Tracksuit ya blue yenye mistari mieupe 1.
- ❖ Bukta 2 za rangi ya blue na raba za michezo jozi 2

KIAMBATISHO B; SHERIA ZA SHULE (UNATAKIWA UZISOME NA UZIELEWE VEMA)

SHERIA ZA SHULE AMBAZO LAZIMA UZIZINGATIE.

1. HESHIMA

- ❖ Unatakiwa uoneshe heshima kwa Walimu, Wazazi, Walezi, Wageni na Wanafunzi wenzako.
- ❖ Mwalimu anapopita mwanafunzi asimame na kusalimia kwa lugha ya kiingereza.
- ❖ Ni mwiko kwa mwanafunzi kutumia lugha ya kihuni au matusi.
- ❖ Unatakiwa kuiheshimu bendera ya Taifa, nembo ya Taifa, Picha ya Raisi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Katiba ya Nchi.

2. UTII

- ❖ Mwanafunzi atakuwa mtii kwa Walimu, Wazazi, Walezi, Wageni, Viranja wa shule na wanafunzi wenzake.
- ❖ Mwanafunzi atatakiwa kutii kengele ya shule.
- ❖ Mwanafunzi atatekeleza amri ya Mwalimu bila ubishi.
- ❖ Mwanafunzi atatakiwa kufuata ratiba ya Shule Kama ilivyopangwa.
- ❖ Mwanafunzi hatakiwi kuzurura usiku, mwisho wa kuonekana mtaani ni saa 1:00 usiku

3. SEHEMU ZILIZOKATAZWA

- ❖ Guest House na kumbi za starehe.
- ❖ Sehemu za kuuzia pombe.
- ❖ Sehemu za kuchezea pool na kamari.
- ❖ Nyumba za Walimu.
- ❖ Ofisi za Walimu isipokuwa kwa kibali.
- ❖ Maabara isipokuwa kwa kibali.

4. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UKAFUKUZWA SHULE

1. Wizi
2. Uasherati na Ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya Madawa ya kulevya Kama vile uvutaji Bangi, Mirungi, Cocaine.
5. Kupiga au kupigana
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma

7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kupata/kusababisha mimba au kuharibu mimba ndani au nje ya shule
10. Kugoma, kuchochea na kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
11. Kukataa adhabu kwa makusudi
12. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi.

KIAMBATISHO C: HISTORIA YA MWANAFUNZI

1. JINA LA MWANAFUNZI(MAJINA MATATU).....
 2. MAJINA YA BABA MZAZI/MLEZI.....
 3. MAJINA YA MAMA MZAZI/MLEZI
 4. SHULE YA MSINGI ALIYOTOKA.....
 5. NAMBARI YA MTIHANI.....
 6. JINSI: ME/KE
 7. KABILA URAIA.....DINI/DHEHEBU.....
 8. TAREHE YA KUZALIWA.....UMRI.....
 9. MICHEZO UNAYOPENDA SHULENI.....
 10. KAZI ZA MIKONO UNAZOPENDA KUFANYA SHULENI.
 11. MAHALI/KIJJI UNACHOISHI SASA.....
- SAINI YA MWANAFUNZI. TAREHE.....

KIAMBATISHO D: KIAPO CHA MWANAFUNZI KUFUATA SHERIA ZA SHULE NA KUTOSHIRIKI WALA KUANZISHA MIGOMO (IJAZWE MBELE YA MKUU WA SHULE)

Mimi..... ambaye nimechaguliwa kuijunga shule ya Sekondari Mwisi 2020, Naapa kuwa nitafuata sheria za Shule na sitashiriki wala kuanzisha mgomo wa aina yoyote kwa muda wote nitakao kuwepo shuleni. Endapo nikivunja sheria za Shule naomba adhabu Kali ichukuliwe dhidi yangu.

Ewe Mola wangu nisaidie.

.....
Tarehe.

KJAMBATISHO E: KIAPO CHA MZAZI KATIKA KUSHIRJKI NA KUTIMIZA MAJUKUMU YAKE KWA MWANAFUNZI NA SHULE

(IJAZWE MBELE YA MKUU WA SHULE)

Mimi ambaye ni mzazi/mlezi wa
mwanafunzi Naapa kuwa nitashiriki katika shughuli
zote zinazohusu maendeleo ya kitaaluma ya kijana wangu na nitatimiza majukumu yangu Kama
mzazi kwa kijana wangu na Shule pia.

Nimezisoma sheria na taratibu zote za shule hii na nina ahidi kuzifuata. Endapo sitatimiza
majukumu yangu Kama mzazi/mlezi naomba sheria ichukuliwe dhidi yangu.

Ewe Mola wangu nisaidie.

.....

Tarehe.

KIAMBATASHO F: HOSPITALI (IJAZWE HOSPITALINI)

PRESIDENT'S OFFICE REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT

**MWISI SECONDARY SCHOOL,
P.O.BOX 173,
IGUNGA.
DATE.....**

Ref No

The medical officer (government hospital)

.....
.....

PART A: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

Mr/Mrs. Miss(Name in full).
Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full-time
secondary education.

The examination should include the following ineligible in case of defect; pregnancy (category 4)
will also render a girl ineligible for secondary Education.

1. (a) Eye sight (b) speech (c) Hearing (d) Limb (e) Venereal diseases (f) Leprosy
(g) Epilepsy
2. Neuroses
3. Other serious diseases

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

1. (a) Eye sight.....
- (b) Speech.....
- (c) Hearing.....
- (d) Limb.....

(e) Venereal diseases.....

(f) Leprosy.....

(g) Epilepsy.....

2. Neuroses.....

3. Other serious diseases.....

4. Pregnancy.....

I have examined the above named and consider that he/she is physically fit/unfit for a full -time secondary education.

Designation..... Date.....

.....
Name and signature & official stamp

(To be completed by a government officer)